



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA



**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA MUDA ZA WASIMAMIZI WA VITUO VYA  
UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA MWAKA 2024 UTAKAOFANYIKA TAREHE  
27 NOVEMBA 2024.**

Kwa madhumumi ya usimamizi wa vituo vya upigia kura kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa Mwaka 2024 na kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 7(1) ya Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji Tangazo la Serikali Na.571 na Kanuni 6(1) ya Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji Tangazo la Serikali Na.572 Mamlaka za Miji Midogo za Mwaka 2024, Msimamizi wa Uchaguzi anakaribisha maombi kutoka kwa **watumishi wa umma** wenye weledi, waadilifu, walioshiriki mazoezi ya kitaifa na wenye uzoefu wa shughuli za uchaguzi kujaza nafasi za **Msimamizi wa Kituo** na **Msimamizi Msaidizi wa kituo**.

**A. SIFA ZA MWOMBAJI WA NAFASI YA USIMAMIZI WA KITUO**

- i. Awe raia wa Tanzania na mtumishi wa umma.
- ii. Awe hajawahi kutuhumiwa au kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwa makosa ya uadilifu na uwajibikaji katika utumishi wa umma.
- iii. Awe mwadilifu na mtiifu.
- iv. Awe tayari kufanya kazi kwa kuzingatia masharti ya ajira.

**B. MALIPO**

- i. Kwa siku za Semina/mafunzo atalipwa posho ya shilingi 30,000 kwa siku na nauli shilingi 10,000.00
- ii. Siku ya uchaguzi atalipwa posho ya shilingi 30,000 na Nauli shilingi 10,000.00 kwa muda wa siku mbili.

**C. MASHARTI YA JUMLA**

Mwombaji lazima awe mtumishi wa umma na aainishe nafasi anayoomba pamoja na Kata au Kijiji atakachofanyia kazi.

Uk.1



Barua zote zitumwe kwa Msimamizi wa Uchaguzi Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba na zitapokelewa kwenye ofisi za Watendaji wa Kata kwa niaba ya Msimamizi wa Uchaguzi.

Watendaji wa Kata watalazimika kuwasilisha kwa Msimamizi wa Uchaguzi orodha ya waombaji wote pamoja na barua halisi za waombaji **kabla au ifikapo tarehe 10 Novemba, 2024 saa 4:00 asubuhi.**

**Orodha ya watakaoteuliwa kusimamia uchaguzi vituoni itatolewa tarehe 20 Novemba 2024.**

Tangazo limetolewa na;



Dr. Amon D. Mkoga

**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI,  
HALMASHAURI YA WILAYA KWIMBA.**



Serikali za Mitaa, Sauti ya Wananchi,  
**Jitokeze Kushiriki Uchaguzi**

**Nakala:**

**Mbao zote za matangazo na tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba – [www.kwimbadc.go.tz](http://www.kwimbadc.go.tz)**

**04 Novemba, 2024.**

Uk.1